مجلة العلوم الإنسانية
**Journal of Human Sciences**
www.Suj.sebhau.edu.ly
Received 20/04/2017 Revised 08/12/2017 Published online 01/01/2018

# Mfumo Wa Elimu Na Hali Ya Lugha Ya Kiswahili Nchini Libya

Ibrahim Elhadi Mohamed
IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA KIAFRIKA, KITIVU CHA SANAA, CHUO KIKUU CHA SEBHA, Libya

**MUHTASARI** Makala hii imejadili suala la Mfumo Wa Elimu na Hali ya Lugha ya Kiswahili Nchini Libya, Katika makala hii tumetoa taarifa kuhusu mfumo wa elimu kwa jumla na nafasi ya lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Libya. Pia tumejadili kwa urefu historia ya Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Sebha na hasa Sehemu ya Kiswahili. Hali kadhalika Jitihada na Ustahiki wa Kiswahili na Sababu za Ustahiki wa Kiswahili umejadiliwa kwa kina katika makala hii.

**الملخص** يناقش هذا البحث النظام والمسارالتعليمي المتبع في الدولة الليبية باالأظافة الى وضع اللغة السواحيلية في ليبيا. أوضح الباحث في بحثه الهيكلية التي يقوم عليها نظام التعليم في ليبيا بصورة عامة.

كما قام الباحث بمناقشة وظع اللغة السواحيلية بشئ من التفصيل من خلال اعطاء نبذة عن قسم اللغات والدراسات الافريقية بجامعة سبها وخاصة قسم اللغة السواحيلية كما تمت مناقشة الحضوة والمكانة التي وصلت اليها اللغة السواحيلية في ليبيا.

## UTANGULIZI WA JUMALA

Kujifunza lugha za kigeni ni moja ya masuala muhimu zaidi ambayo tunashughulikiwa, kupitia utoaji wa utafiti maalumu ambao unaonyesha umuhimu wa kujifunza lugha hizi, hasa lugha za Kiafrika, kama lugha moja ya kigeni ambayo hii inatumika, hususan lugha ya Kiswahili. Ambayo tumejitoa kwa makala hii kwa ajili ya kueleza mfululizo wa awamu ya mfumo wa elimu nchini Libya kwa jumla, pia tutaleza nafasi ya lugha ya Kiarabu, lugha za Kigeni na lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Libya. Kama tutajadili na tutafafanua historia ya Idara ya lugha na Taaluma za Kiafrika katika chuo kikuu cha sebha kwa upande mbalimbali k.v. malengo ya kuanzisha Idara, muhtasari wa kozi za programu ya Kiswahili, jitihada na ustahiki wa Kiswahili na sababu za ustahiki wa Kiswahili nchini Libya.

## UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha mojawapo kati ya lugha za Kiafrika na ambayo hivi sasa imepata umaarufu mkubwa. Kwa mujibu wa Greenberg (1963) lugha hii imo katika mbari kubwa ya lugha za Kinija-Kordofani. Chini ya *mbari* hii kubwa kuna familia kubwa ijulikanayo kama Nija-Kongo ambayo chini yake kuna familia ndogo ijulikanayo kama Benue-Kongo. Lugha za Kibantu, Kiswahili kikiwemo, ziko chini ya familia hii ya Benue-Kongo. Kwa hivyo, asili ya Kiswahili ni Afrika. Kwa mujibu wa maelezo ya Massamba na wenzie (2001: 2), wanasema:

"Miongoni mwa lugha kuu za Kiafrika ambazo zinazungumzwa na wengi sana ndani na nje ya bara la Afrika ni lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania, Kenya, Uganda na ni lingua-franka katika nchi kama Zambia, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo (Zaire), kaskazini mwa Msumbiji, Malawi na kadhalika."

Ueneaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili duniani unaonekana wazi kwa kiasi kikubwa kutokana na utumiaji wa Kiswahili katika vyombo vya kutangazia habari vya kimataifa. Kuna mashirika mbalimbali yanayotekeleza azma hii, kwa uchache ni kama vile: Redio Ujeremani, Sauti ya Afrika nchini Libya, Shirika la utangazaji la Uingereza (BBC), Sauti ya Marekani, Sauti ya China na Sauti ya Japani. Mashirika hayo na mengine yanatumia Kiswahili kama lugha mojawapo ya kurushia matangazo.Ama, kuhusu upande wa ufundishwaji wa Kiswahili ulimwenguni, Ibrahim Elhadi (2004: 2) anachangia kwa kusema:

"Pamoja na nchi za Afrika Mashariki hususan – Tanzania, Kenya na Uganda – ambako Kiswahili hufundishwa kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu, hivi sasa Kiswahili hufundishwa katika vyuo vikuu mbalimbali ulimwenguni. Mifano michache ifuatayo inathibitisha ukweli wa hoja hii: Chuo Kikuu cha Sebha, nchini Libya; Chuo Kikuu cha Port Harcourt, nchini Nigeria; Chuo Kikuu cha Helsinki, nchini Finland; Chuo Kikuu cha Uppsala, nchini Sweden; Chuo Kikuu cha Warsaw, nchini Poland; Chuo Kikuu cha Khartoum, nchini Sudan; Chuo Kikuu cha Legon, nchini Ghana; Chuo Kikuu cha Leiden, nchini Uholanzi; Chuo Kikuu cha Ain Shams, nchini Misri; Chuo Kikuu cha Osaka, nchini Japani; Chuo Kikuu cha London (SOAS), nchini Uingereza; na Chuo Kikuu cha Meksiko nchini Meksiko."

Kwa upande wa bara la Afrika, zimekuweka harakati za kuanzisha Umoja wa Afrika zilizoendeshwa na Libya. Katika harakati hizo, moja kati ya azma zinazokusudiwa na Libya ni kutoa nafasi maalumu kwa lugha za Kiafrika, hususan Kiarabu, Kiswahili, Kihausa na Kifulani *kama lugha rasmi* za Umoja huo wa Afrika. Ni dhahiri kwamba hili ni mojawapo ya changamoto kubwa kwa lugha hizi za Kiafrika, hususan lugha ya Kiswahili.Kwa mantiki hiyo, Libya iliamua mapema kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Libya.

## Mfumo wa Elimu Nchini Libya

Serikali ya Mapinduzi ya Libya ilishughulikia mfumo wa elimu endelevu ambao ulijengwa kwa sera madhubuti. Lengo lake ni kumjenga mwanadamu (Mlibya) ili awe nguzo kuu na mwenye sifa zinazostahiki kushiriki kwenye ujenzi

wa nchi yake. Sera ilimtaka, kila Mlibya apewe haki ya kupata elimu; haki hii iwe ya lazima kwa kila Mlibya mpaka mwisho wa elimu yake ya msingi ambayo ni ya miaka tisa (9). Serikali iliutambua umuhimu wa sera hii na ikawa mdhamini wa kila mtoto wa Kilibya katika kutekeleza hatua zote za elimu yake ambayo ni ya bure kwa kila mtoto. Ufuatao ni muhtasari wa awamu mbalimbali katika mfumo wa elimu nchini Libya:

**Awamu ya Elimu ya Msingi**

Awamu hii ni ya lazima kwa kila mtoto nchini Libya. Muda wa awamu ya elimu ya msingi ni miaka tisa. Aghalabu watoto wanaojiunga na awamu hii ni wale ambao wametimiza umri wa miaka sita. Awamu hii inagawanywa katika sehemu mbili:

**Sehemu ya Kwanza ya Awamu ya Elimu ya Msingi**

Awamu hii muda wake ni miaka sita. Wanafunzi wanajifunza misingi ya lugha ya Kiarabu na Kiingereza, Dini, Kusoma na Kuandika, Hisabati, Sayansi, Historia, Jiografia, Kompyuta na Uchoraji.

**Sehemu ya Pili ya Awamu ya Elimu ya Msingi**

Muda wa awamu hii ni miaka mitatu. Madhumuni yake ni kutaka kujua kipaji cha kila mwanafunzi kiakili na kuweza kukiimarisha ili afikiapo mwisho wa mwaka wa tatu, uongozi uweze kuamua mchepuo muafaka kwa kila mwanafunzi kulingana na mahitaji ya jamii.

**Awamu ya Elimu ya Shule za Upili (Sekondari)**

Wanafunzi wanaopata Cheti cha Kumaliza Elimu ya Msingi ndio wanaokubaliwa kujiunga katika Awamu hii ya Elimu ya Shule ya Upili (Sekondari). Katika mfumo wa elimu ya Sekondari , wanafunzi wanapewa fursa ya kuchagua kati ya mchepuo wa Sanaa na mchepuo wa Sayansi. Masomo yanayofundishwa katika mchepuo wa Sanaa ni: Historia, Jiografia, Falsafa na Jamii. Masomo yanayofundishwa katika mchepuo Sayansi ni: Fizikia, Kemia, Bayolojia na Hisabati. Wanafunzi wanaofaulu katika mitihani hii hutunukiwa Cheti cha Elimu ya Sekondari.

**Awamu wa Elimu ya Chuo Kikuu na Juu**

Mfumo wa Elimu ya Chuo Kikuu na Juu nchini Libya umegawanywa katika awamu mbili: kwanza, Awamu ya Mfumo wa Elimu ya Chuo Kikuu; Pili, Awamu ya Mfumo wa Elimu ya Juu. Mfumo wa Elimu ya Chuo Kikuu ni ule unaofundisha kozi za Shahada ya Kwanza tu, lakini Mfumo wa Elimu ya Juu ni ule unaofundisha kozi za Shahada ya Pili ( Uzamili ) na Shahada ya Tatu ( Uzamivu ). Vyuo Vikuu vyote nchini Libya vinaweza kufundisha kozi za Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu kutegemeana na uwezo wa Chuo Kikuu husika.

Jumla ya vyuo vikuu nchini Libya ni kumi na nne (14), navyo ni: Chuo Kikuu cha Tripoli, mjini Tripoli; Chuo Kikuu cha Benghazi, mjini Benghazi; Chuo Kikuu cha Sebha, mjini Sebha; Chuo Kikuu cha Omar Al Mukhtar, mjini Baydha; Chuo Kikuu cha Sirt, mjini Sirt; Chuo Kikuu cha Al Zawia, mjini Al Zawia; Chuo Kikuu cha Al Asmaria, mjini Zlitin na Chuo Kikuu cha Aljabal Algharbi, mjini Gharyan; Chuo Kikuu cha Al Arab Altubiya, mjini Bengazi; Chuo Kikuu cha Misurata, mjini Misurata; Ufafanuzi wa kina wa Elimu ya Chuo Kikuu na Elimu ya Juu ni kama ifuatavyo:

**Awamu ya Elimu ya Chuo Kikuu**

Wanafunzi wanaojiunga Awamu ya Elimu ya Chuo Kikuu ni wale waliomaliza Awamu ya Elimu ya Shule za Sekondari. Serikali ya Libya ilizingatia umuhimu wa Elimu ya Chuo Kikuu mara tu baada ya awamu ya Elimu ya Sekondari. Kwa hivyo, ikaanzisha Vyuo Vikuu vingi nchini ili kufanikisha mahitaji ya jamii ya kupata wananchi wenye uwezo kwenye nyanja mbalimbali za elimu. Vyuo Vikuu na Taasisi zimeenea katika sehemu zote nchini Libya.

Mfumo wa masomo katika vitivo vya vyuo vikuu nchini Libya unatofautiana kati ya Kitivo kimoja na kingine, baadhi ya vyuo hivyo vinafuata mfumo wa programu ya mwaka mmoja mmoja (mwaka mzima) kwa mfululizo wa miaka mine. Mwanafunzi anayehitimu, hupewa Shahada ya Kwanza. Vitivo vingine vinafuata mfumo wa programu ya kozi. Katika programu hii, mwanafunzi hutakiwa kutimiza vigezo mia moja na thelathini ( vigezo 130) ndipo atunukiwe Shahada yake. Ama, kuhusu Vitivo vya Tiba, mfumo unaofuatwa ni ule wa programu ya mwaka mmoja mmoja kwa mfululizo wa miaka sita (6). Mwanafunzi anayefaulu hutunukiwa Shahada ya Kwanza katika taaluma ya Tiba.

**Awamu ya Elimu ya Juu**

Serikali ya Libya imeamua kuvipa vyuo vikuu, taasisi na vyuo vya elimu ya juu Majukumu ya kuboresha elimu ya Chuo Kikuu na kuwaandaa wataalamu wa kufundisha na wa kufanya utafiti. Aidha, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi kusoma nje ya nchi ili wajipatie elimu katika nyanja mbalimbali hususan, zile nyanja ambazo hazipatikani katika vyuo vikuu nchini Libya.

**Nafasi ya Lugha Katika Mfumo wa Elimu Nchini Libya:**

**Nafasi ya Kiarabu**

Nchini Libya, lugha ya Kiarabu ndiyo iliyopewa kipaumbele katika utamaduni wa Walibya. Kiarabu ni ***lugha rasmi*** ya Taifa la Walibya. Walibya wote, ambao idadi yao ni takribani milioni sita (6,000,000) huzungumza Kiarabu. Kiarabu wanachozungumza na Walibya ni lahaja mojawapo tu, kati ya lahaja kadhaa za Lugha ya Kiarabu Sanifu ambacho, aghalabu husomwa katika Kitabu kitakatifu cha Kur'an. "Kiarabu" kinachozungumzwa na Waarabu wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani ni lahaja mbalimbali za Kiarabu kilichotumika katika Kur'an.

Katika mfumo wa elimu nchini Libya, Kiarabu, sayansi na Kur'an, husomeshwa kuanzia Awamu ya Shule za Msingi hadi kwenye Awamu ya Elimu ya Juu.

**Nafasi ya Lugha za Kigeni Nchini Libya:**

**Nafasi ya Lugha za Kigeni Zitokazo Nje ya Bara la Afrika Nchini Libya**

Licha ya Kiarabu lugha zingine zinazofundishwa nchini Libya ni Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani na Kiitaliano. Hizi ni 'lugha za kigeni' kwa maana halisi ya 'lugha za kigeni' kwa sababu wenye lugha hizi ni wenyeji wa nchi za Bara la Yuropa: Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Italia, nchi ambazo ziko nje ya Bara la Afrika. Lugha hizi hufundishwa kwa bidii nchini Libya, hususani Kiingereza, kwa sababu ya umaarufu wake ulimwenguni katika taaluma ya Sayansi na Teknolojia.

**Nafasi ya Lugha za Kigeni Nchini Libya Zitokazo Ndani ya Bara la Afrika**

Lugha za kigeni nchini Libya zitokazo ndani ya Bara la Afrika na ambazo husomeshwa nchini Libya ni Kiswahili, Kihausa na Kifulani. Kati ya hizi, Kiswahili ndicho kinachoshika nafasi ya kwanza katika kupata wanafunzi wengi madarasani. Kwa hivyo, Kiswahili kimepewa nafasi maalumu katika mfumo wa Elimu nchini Libya.

**Nafasi ya Kiswahili Katika Mfumo wa Elimu Nchini Libya**

Ufundishaji wa Kiswahili ni kipengele kimojawapo ambacho tayari kimekwishaanza kuingizwa katika mfumo wa elimu nchini Libya. Uamuzi huu umetolewa kutokana na umaarufu wa Kiswahili, si katika nchi za Bara la Afrika tu, bali pia katika mabara mengine duniani, hususani Bara la Yuropa, Marekani (Kaskazini na Kusini) na Asia.

Kwa mujibu wa Kihore, Y.M ( 2000 ) Kiswahili ambacho huzungumzwa katika Afrika Mashariki kinakuwa kiungo muhimu cha mawasiliano baina ya Waswahili na Waarabu, au Waswahili na Waafrika Magharibi, au Waswahili na Waafrika Kusini.

Taib, A.H. (2009) anadai kwamba lengo kubwa la kutoa nafasi kwa Kiswahili katika mfumo wa Elimu nchini Libya ni kukiwezesha Kiswahili kitumike katika Umoja wa Afrika sambamba na hizo lugha zingine, hususani katika muktadha wa Ki-Diplomasia na Biashara. Aidha, ni kukiwezesha Kiswahili pamoja na lugha hizo zingine kupata nafasi ya kufundishwa, si kama somo tu, bali pia Kiswahili kiwe lugha mojawapo katika Taaluma ya Tafsiri.

**Historia Fupi ya Idara ya Lugha naTaaluma za Kiafrika Katika Chuo Kikuu cha Sebha Nchini Libya**

Katika mwaka 1984, kulitangazwa rasmi kwamba Lugha za Kiafrika zifundishwe nchini Libya. Kutokana na uamuzi huo, Wizara ya Elimu ya Juu ilipewa majukumu ya kuanzisha Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika katika Kitivo cha sanaa cha chuo kikuu nchini Libya. Katika Kitivo cha Sanaa cha Chuo Kikuu cha Sebha, Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika iliamua kufundisha lugha zifuatazo ambazo kila mojawapo ilitengewa Sehemu yake:

1. Sehemu ya Kiswahili
2. Sehemu ya Kihausa
3. Sehemu ya Kifulani

**Sehemu ya Kiswahili**

**Awamu ya Kwanza ya Utekelezaji wa Masomo ya Kiswahili [1984-1987]**

Kiswahili kilianza kufundishwa mwaka 1984 katika Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Sebha kwa mfumo wa masomo ya muhula. Kwa mujibu wa mfumo huu, wanafunzi walitakiwa kusoma mihula sita. Aidha, wanafunzi walitakiwa kupelekwa nchini Tanzania ambako walikaa kwa muda wa miezi sita wakijumuika na wenyeji wao Waswahili wa Watanzania ili waupate muktadha muafaka wa kujizoesha kukizungumza na kukiandika Kiswahili.

**Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Masomo ya Kiswahili [1988 – na kuendelea ]**

Ulipofikia mwaka wa masomo [1988 -1989], mfumo wa masomo ulibadilishwa: badala ya Mfumo wa Masomo ya muhula, ukawa mfumo wa masomo ya mwaka kwa muda wa miaka minne.

**MUHTASARI WA KOZI ZA PROGRAMU YA KISWAHILI**

Ili kufanikisha majukumu ya ufundishaji wa Kiswahili katika Idara ya lugha na taaluma za Kiafrika,Idara ilichukua hatua kutayarisha muhtasari wa kozi za programu ya Kiswahili.

**KOZI ZA MUHULA WA KWANZA ( I )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 101 : MAZUNGUMZO | 4 | Mwanafunzi aweze kuamkia , kujitambulisha na kueleza shughuli zake za kila siku katika mazungumzo . |
| SW 102 : UFAHAMU | 4 | Mwanafunzi aweze kujenga msamiati wa nyanja mbalimbali na kujibu maswali rahisi ya ufahamu . |
| SW 103 : MAABARA YA LUGHA | 2 | Mwanafunzi aweze kusikilza, kutamka kwa usahihi sauti , maneno na sentensi fupifupi za Kiswahili . |
| SW 104 : KUSOMA NA KUANDIKA | 4 | Mwanafunzi aweze kujua abjadi ya Kiswahili kwa jumla na Kuandika herufi zake kwa hati ya Kirumi kwa unadhifu |
| SW 105 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua na kutumia Viwakilishi nafsi,Vitenzi vya msingi,Viulizi na Vimilikishi katika Mazungumzo ya kuamkia na utambulisho. |

**KOZI ZA MUHULA WA PILI ( II )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 201 : MAZUNGUMZO | 4 | Mwanafunzi aweze kumudu mazungumzo akitumia nyakati mbalimbali , katika mazingira yanayomzunguka anapokutana na watu wengi. |
| SW 102 : UFAHAMU | 4 | Mwanafunzi aweze Kusoma makala fupi na kujibu maswali juu yake . |
| SW 203 : MAABARA YA LUGHA | 2 | Mwanafunzi aweze kutamka maneno maalumu kwa usahihi pamoja na kusema kwa usahihi tungo - sentensi za viwango mbalimbali za Kiswahili . |
| SW 204 : KUSOMA NA KUANDIKA | 4 | Mwanafunzi aweze kukamilisha ujuzi wake wa kusoma na kuandika maneno ya Kiswahili yenye herufi H-Z . |
| SW 205 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kutumia Vitenzi katika nyakati mbalimbali katika kukubali na kukanusha , katika Umoja na Wingi na pia aweze kuzingatia kanuni za vitenzi vya silabi moja na kauli chache za sentensi . |

**KOZI ZA MUHULA WA TATU ( III )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 301 : MAZUNGUMZO | 4 | Mwanafunzi aweze kumudu mazungumzo katika mazingira ya shughuli mbalimbali , kueleza jinsi kitu kilivyo au kilipo , mavazi mbalimbali na vyakula mbalimbali . |
| SW 302 : UFAHAMU | 2 | Mwanafunzi aweze kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma au kusikia .Pia aweze kuifasili alivyoielewa na kuifupisha . |
| SW 303 : UTUNGAJI | 2 | Mwanafunzi aweze kutumia msaada atakaokuwa amepewa kukamilisha kazi anayotakiwa kutunga |
| SW 304 : KUSOMA NA KUANDIKA | 4 | Mwanafunzi aweze kusoma na kuandika kwa upesi na kwa usahihi hadithi , habari na makala fupi |
| SW 305 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua aina /kategoria za maneno ya Kiswahili na kuchambua Nomino na Vivumishi vya Kiswahili |

**KOZI ZA MUHULA WA NNE ( IV )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 401 : MAZUNGUMZO | 4 | Mwanafunzi aweze kujieleza kwa ufasaha katika kueleza matukio . |
| SW 402 : UFAHAMU | 2 | Mwanafunzi aweze kusoma na kuelewa makala zilizo na semi maalumu kv.methali, vitendawili, nahau n.k . |
| SW 403 : UTUNGAJI | 2 | Mwanafunzi aweze kuwa mbunifu na kukamilisha Utungaji wake kwa msaada mdogo sana . |
| SW 404 : KUSOMA NA KUANDIKA | 4 | Mwanafunzi aweze kupenda kusoma na kuandika kutokana na tabia ya kuweka kumbukumbu ya yale anayosoma na kuandika |
| SW 405 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua upatanisho wa kisarufi Kati ya Nomino na Vivumishi na pia Vitenzi pamoja na Dhana ya Urejeshi . |

**KOZI ZA MUHULA WA TANO ( V )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 501 : FONETIKI | 3 | Mwanafunzi aweze kujua Fonetiki ni nini na dhima yake katika taaluma ya Isimu . |
| SW 502 : UTANGULIZI WA FASIHI | 2 | Mwanafunzi aweze kujua maana ya Fasihi , chimbuko na tanzu zake pamoja na dhima yake . |
| SW 503 : TAFSIRI | 3 | Mwanafunzi aweze kujua tafsiri kama taaluma na aizingatie misingi yake anapofasiri . |
| SW 504 : UTUNGAJI | 2 | Mwanafunzi aweze kuandika insha za mjalada au za kutoa maoni |
| SW 505 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua utumiaji sahihi wa Viambishi Mtendwa katika kitenzi na pia Kauli za Kitenzi . |

**KOZI ZA MUHULA WA SITA ( VI )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 601 : FONOLOJIA YA KISWAHILI | 3 | Mwanafunzi aweze kubainisha utamkaji wa irabu na pia kuhusisha Fonolojia kwa kutumia lugha ya Kiswahili . |
| SW 602 : FASIHI | 2 | Mwanafunzi aweze kufahamu tanzu zaidi za Fasihi Simulizi na matumizi yake . |
| SW 603 : HISTORIA YA KISWAHILI | 2 | Mwanafunzi aweze kujua asili ya lugha ya Kiswahili , kwa nini Kiswahili ni lugha ya Kibantu na kukua kwake katika karne mbalimbali. |
| SW 604 : MATUMIZI YA LUGHA | 3 | Mwanafunzi aweze kupata hazina ya kutosha kwa ajili ya kutumia Kiswahili kulingana na mazingira au shughuli mbalimbali. |
| SW 605 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua kwa undani aina zaidi za maneno , unyambulishaji wa maneno na uundaji wa maneno . |

**KOZI ZA MUHULA WA SABA ( VII )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 701 : HISTORIA YA KISWAHILI | 3 | Mwanafunzi aweze kujua maendeleo ya Kiswahili tangu wakati wa harakati za kutafuta uhuru mpaka leo hii . |
| SW 702 : FASIHI | 3 | Mwanafunzi aweze kujua misingi ya Fasihi Andishi na jinsi ya kuihakiki . |
| SW 703 : TAFSIRI | 2 | : Mwanafunzi aweze kutumia misingi ya Tafsiri kufasiri kazi mbalimbali . |
| SW 704 MATUMIZI YA LUGHA | 4 | : Mwanafunzi aweze kujua tofauti kati ya Lugha ya Mazungumzo na Lugha ya Maandishi , chanzo cha makosa ya matumizi ya maneno na matumizi ya kamusi . |
| SW 705 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi aweze kujua maana ya Sintaksia (Sarufi Miundo) na viwango vyake katika taaluma ya Sarufi |
| SW 706 : MBINU ZA UTAFITI | 2 | Mwanafunzi aweze kujua misingi mikuu ya utafiti na dhima yake katika kazi ya utafiti . |

**KOZI ZA MUHULA WA NANE ( VIII )**

| KOZI | SAA KWA WIKI | MADHUMUNI YA KOZI |
|---|---|---|
| SW 801 : UTAMADUNI | 3 | Mwanafunzi aweze kujua vitambulisho vikuu vya Waswahili katika maisha yao ya siku kwa siku |
| SW 802 : FASIHI | 2 | Mwanafunzi aweze kujua muundo wa mashairi ya Kiswahili na kuyachambua . |
| SW 803 : TAFSIRI | 3 | Mwanafunzi aweze kutumia misingi ya Tafsiri kufasiri kazi mbalimbali . |
| SW 804 MATUMIZI YA LUGHA | 2 | Mwanafunzi aweze kujenga msamiati / istilahi za nyanja mbalimbali, kujua dhima ya ishara katika mawasiliano na kutumia hazina hiyo katika stadi za midahalo |
| SW 805 : SARUFI | 4 | Mwanafunzi ajue taaluma ya Semantiki kama tawi la isimu na dhima yake katika lugha |
| SW 806 : UTAFITI | 2 | Mwanafunzi aweze Kuandika kwa unadhifu kazi maalumu kutokana na Utafiti aliofanya |

**(*Chanzo:Idara ya lugha, Chuo kikuu cha Sebh)***

**Hali ya Uhitimu**

Tangu kuanzishwa kwake, Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika imefanikiwa kuhitimisha wanafunzi wa Kiswahili kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| | Mwaka wa Kutunukiwa Shahada ya B.A. | Idadi ya Wanafunzi (Wahitimu) |
|---|---|---|
| 1 | 1986-1987 | 10 |
| 2 | 1987-1988 | 12 |
| 3 | 1990-1991 | 25 |
| 4 | 1991-1992 | 15 |
| 5 | 1992-1993 | 6 |
| 6 | 1993-1994 | 1 |
| 7 | 1994-1995 | 7 |
| 8 | 1995-1996 | 1 |
| 9 | 2001-2002 | 4 |
| 10 | 2002-2003 | 3 |
| 11 | 2003-2004 | 11 |
| 12 | 2004-2005 | 8 |
| 13 | 2005-2006 | 13 |
| 14 | 2006-2007 | 9 |
| 15 | 2007-2008 | 10 |
| 16 | 2008- 2009 | 18 |
| 17 | 2009- 2010 | 12 |
| 18 | 2010- 2011 | 14 |
| 19 | 2011- 2012 | 6 |
| 20 | 2012- 2013 | 25 |
| 21 | 2013- 2014 | 13 |
| 22 | 2014- 2015 | 5 |
| 23 | 2015- 2016 | 3 |
| 24 | 2016- 2017 | 3 |

**(*Chanzo: Idara ya lugha, Chuo kikuu cha Sebh)***

**Malengo ya Kuanzisha Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika**

Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika inalenga kufanikisha malengo mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Kufundisha lugha za Kiafrika na Fasihi zake.
2. Kukuza utafiti katika masuala yanayolihusu Bara la Afrika.
3. Kuanzisha uhusiano mwema wa ushirikiano wa kitaaluma na uratibu wa vyuo vya Kiafrika kwa kuiunganisha idara na njia za kisasa za teknolojia ya habari.
4. Kuwaandaa watumishi wa kijamii, kiuchumi na wanadiplomasia wa kisiasa wa kesho ili waweze kutoa mchango wao katika kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na ya kisiasa ndani ya bara hili.
5. Kukiandaa kizazi cha kesho chenye maarifa na kujiamini ili kujenga na kulinda Bara hili dhidi ya vitisho vilivyopo na vinavyoweza kutokea.
6. Kutoa ushauri kwa idara za serikali na sekta zake katika nyanja mbalimbali.
7. Kutoa msaada na uelekeze kwa serikali na sekta binafsi zinazojishughulisha na masuala ya Afrika.
8. Kuwaandaa wakufunzi wa walimu kwa ajili kufundisha mitaala ya lugha za Kiafrika iliyoandaliwa kwa ajili ya viwango mbalimbali vya Awamu ya Elimu ya Msingi.

**Jitihada na Ustahiki wa Kiswahili Nchini Liby**

Kwamba Kiswahili kina kila haki ya kuwa na ustahiki si katika Jamii ya Walibya tu, bali pia katika jamii yoyote ya binadamu wanaopenda maendeleo ya binadamu wengine kwa ujumla; kwani *lugha* ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya jamii ya binadamu wakati wote katika historia yake ya kuumbwa na kuishi duniani. Kwa mantiki hii, jamii ya Walibya na uongozi wao, wameamua kufanya jitihada katika kukieneza na katika kukiendeleza Kiswahili nchini Libya, kama ifuatavyo:

**Jitihada za Kueneza na Kuendeleza Kiswahili Nchini Libya**

Nchini Libya uamuzi maridhawa umechukuliwa ili kueneza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Ili kukieneza, Serikali ya Libya iliamua kukifundisha Kiswahili nchini. Hatua zilizochukuliwa ni kukifundisha katika ngazi za shule za Sekondari, Vyuo na Vyuo vikuu.

Ili kukiendeleza Kiswahili, Serikali ya Libya:

(a) Ilitoa fursa kwa waandishi wenyeji na wageni kujitokeza kuvitayarisha vitabu vya kiada vya Kiswahili kwa viwango mbalimbali.
(b) Huwasafirisha wanafunzi wa Chuo Kikuu mpaka Tanzania wakasome wakati wa kipindi cha mwaka wa mwisho masomo yao.
(c) Hutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaomalizia masomo yao ya Chuo Kikuu nchini Tanzania ili kupata Shahada ya Uzamili au Shahada ya Uzamivu.

Azma ya hatua zote hizi ni kuchangia katika kufanikisha mahitaji ya kukieneza na kukiendeleza Kiswahili nchini Libya. Ijapokuwa uamuzi wa kufundisha na kueneza Kiswahili umechukuliwa tangu muda mrefu, lakini makongamano na semina zilianza kuendeshwa miaka michache tu iliyopita.

Mnamo mwaka wa 2009 [ tarehe 15/4/2009 ], Chuo Kikuu cha Sebha kilisherehekea

maadhimisho ya robo karne ya kufundisha Kiswahili, na kwenye siku ya maadhimisho, makala mengi yaliyotolewa katika Semina hiyo, yaliandikwa kwa Kiswahili.

**Ustahiki wa Kiswahili Nchini Libya**

Kama tunavyojua, Kiswahili kimeenea mahali pengi ulimwenguni. Libya ni mojawapo ya nchi za Kiarabu ambayo ni maarufu sana si katika Bara la Afrika tu, bali pia katika nchi za Kiarabu kwa ujumla. Utetezi wake kuhusu ustahiki wa Kiswahili nchini Libya una mashiko zaidi kuliko kinavyostahiki katika nchi nyingine yoyote ulimwenguni iliyoko nje ya Bara la Afrika.

**Sababu za Ustahiki wa Kiswahilinchini Libya**

Zipo sababu nyingi zenye mashiko zinazoashiria ustahiki wa Kiswahili nchini Libya; na kwa hiyo, kukifanya Kiswahili kistahiki mno kufundishwa nchini Libya. Libya ni nchi ya Kiarabu ambayo imo barani Afrika.

**Sababu za Kijiografia**

Libya ni nchi ya Kiarabu ambayo imo barani Afrika. Sababu hii ya kijiografia ambayo ina mashiko, inakifanya Kiswahili kistahiki mno kufundishwa nchini Libya kuliko nchi nyingine yoyote, iwe ya Kiarabu au la, iliyoko nje ya Bara la Afrika.

**Sababu za Kimila na Kitamaduni**

Sababu nyingine zinazoashiria ustahiki wa Kiswahili nchini Libya ni kwamba mila na tamaduni za Waswahili zinakaribiana sana na zile za Walibya. Kwa mfano, rahisi wa kujifunza lugha hasa Kiswahili kwenda Kiarabu na Kiarabu kwenda Kiswahili na nyanja nyingine kama starehe na sherehe; harusi, unyago, methali na hadithi.

**Sababu za Kisiasa na Kidiplomasia**

Vile vile, Libya ni nchi ambayo ina uhusiano mzuri sana wa kisiasa, kibiashara na kijamii na nchi nyingi za Kiafrika. Tunashuhudia kuwako kwa ubalozi wa Libya takriban katika kila nchi ya Kiafrika. Kuwepo kwa Walibya wanaoongea Kiswahili kunasaidia utendaji kazi kwa urahisi na ufanisi zaidi katika balozi mbalimbali za Libya barani Afrika.

**HITIMISHO**

Kutokana na tarifa zilizotolewa na zilizochuguzwa katika makala hii matokeo yalikuwa wazi kwamba:

1- Tumetoa picha kuhusu mfumo wa elimu kwa jumla nchini Libya.
2- Tumetoa taarifa kwa upana kuhusu Idara ya lugha na taaluma za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Sebha.
3- Uzingativu na viwango vizuri vilivyofikia hali ya Kiswahili nchini Libya.
**4-** Taarifa zimeonyesha hatua mbalimbali zimechukuliwa kuendeleza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Libya.

**MAREJELEO**


[1]- Greenberg, J, (1963) The Languages of Africa. Ktk. International Journal of American Linguistics, 2.1: II

[2]- Ibrahim, E.M. (2004), Matatizo Ya Matamshi Wanayowapata Wanafunzi Wa Kiarabu Wanapojifunza Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya digirii Ya Uzamili ya M.A.(KiKiswahili) Katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

[3]- Kihore, Y.M ( 2000 ) Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na

[4]- Moja. Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

[5]- Massamba, D.P ( na wenzie) ( 2001) Sarufi Miundo ya Kiswahili sanifu, TUKI

[6]- Taib, A.H. (2009) Mbinu za kufundishia lugha ya Kiswahili kama lugha ya Pili. Makala iliyotolewa katika semina ya kumbukumbu ya kutimiza miaka 25 tangu kuanzishwa kwa idara ya lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Sebha, iliyofanyika tarehe 15 Aprili 2009.

[7]- The research center for African Studies (1) (1988) Proceedings of the conference on:Education for liberation in Africa. Held in Sebha from 20th – 25th March1988.